# MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MACHI, 2021 NA MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2021

Dondoo za tathmini ya Machi, 2021 na mwelekeo wa Aprili, 2021:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Machi, 2021 na mwelekeo wa viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Aprili, 2021 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021 maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalikumbwa na vipindi vya ukavu hususan katika kipindi cha wiki ya kwanza hadi ya tatu, isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria ambayo yalipata vipindi vya mvua.
- Maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yaliendelea kupata mvua za Msimu. Aidha, vipindi vya mvua kubwa pia vimeripotiwa.
- Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021 mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Hata hivyo, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.
- Hali ya joto inatarajiwa kupungua kiasi katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2021.

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021, vipindi vya ukavu vilijitokeza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan katika wiki ya kwanza na ya tatu, isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria ambayo yalipata vipindi vya mvua. Kujitokeza kwa migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na mgandamizo mkubwa wa hewa nchini kulisababisha Ukandamvua wa Kitropiki (ITCZ) kusalia maeneo ya kusini mwa nchi na hivyo kusababisha upungufu wa mvua katika maeneo ya kaskazini. Aidha, ongezeko la

mvua lilijitokeza katika wiki ya nne kwa baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Mvua za Msimu ziliendelea kunyesha katika maeneo mengi katika kipindi cha mwezi Machi,2021. Aidha vipindi kadhaa vya mvua kubwa viliripotiwa katika baadhi ya maeneo. Mnamo tarehe 30 Machi, 2021 kituo cha Lyamungu kilichopo Kilimanjaro kilipima milimita 116.8 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi cha mvua kilichopimwa kwa mwezi Machi, 2021 ikifuatiwa na kituo cha Uyole kilichopima milimita 67.9 mnamo tarehe 07 Machi, 2021 pamoja na kituo cha Mwanza kilichopima milimita 63.8 mnamo tarehe 29 Machi, 2021. Hata hivyo, vipindi vya joto vimeendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo hususan katika ukanda wa pwani.

## 2.0 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA MWEZI APRILI, 2021

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika kipindi chote cha mwezi Aprili, 2021. Aidha, joto la bahari katika eneo la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani. Migandamizo mikubwa ya hewa kusini mwa Afrika inatarajiwa kuimarika kiasi, hivyo kusababisha Ukandamvua wa Kitropiki (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini mwa nchi yetu. Hali ya joto la chini ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuvuma kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2021

Mvua zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo nchini hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2021. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika maeneo yanayopata msimu mmoja mvua kwa mwaka katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi. Mvua za Msimu zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2021. Hata, hivyo upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2021. Hata, hivyo upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Aprili, 2021. Upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya nne ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa mwezi Aprili, 2021. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili, 2021. Upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021. Hata hivyo upungufu unatarajiwa kujitokeza katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo kwa kipindi cha mwezi Aprili 2021. Upungufu wa mvua unatarajiwa hususan wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.3 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2021

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2021 upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.

## 2.4 USHAURI

Katika kipindi cha mwezi Aprili 2021, mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza katika kipindi cha mwezi Aprili, 2021 hivyo, wananchi wanaoishi katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko mara kwa mara au katika mikondo ya maji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Aprili 2021 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz